

HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Mkoa wa Singida

Tel Na: 0262502252/2237

Fax: 0262502719

Email: ded.singidadc@singida.go.tz

S.L.P. 27,
SINGIDA.

Tarehe 22/08/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA WAKIMBIZA MWENGE WA UHURU NGAZI YA MKOA NA WILAYA KWA MWAKA 2023 HALMASHURI YA WILAYA YA SINGIDA.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Singida anawatangazia vijana wote wazalendo wa Wilaya ya Singida uwepo wa nafasi moja (01) ya kukimbiza mwenge wa uhuru Kimkoa mwaka 2023 na nafasi sita (06) za kukimbiza Mwenge wa Uhuru Kiwilaya mwaka 2023.

Sifa za jumla za waombaji

1. Awe raia wa Tanzania na mkazi wa Wilaya ya Singida
2. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 35
3. Awe na afya njema, muadilifu, mchapakazi na mwenye uwezo wa kutunza siri.
4. Awe hajawahi kupatikana na hatia katika makosa ya jinai
5. Atakayeomba nafasi ya kukimbiza mwenge kimkoa awe jinsia ya kike

TARATIBU ZA KUTUMA MAOMBI.

Maombi yawasilishwe katika ofisi za Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Singida au kwa njia ya Posta kwa anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Singida,

S.L.P 27

SINGIDA.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 30/08/2023. Usaili utafanyika Tarehe 01-06/09/2023 saa nne asubuhi katika ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Singida.

Christopher Kidubo

Kny. Mkurugenzi mtendaji

HALMASHAURI YA WILAYA

SINGIDA

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SINGIDA**